# Ufugaji samaki kunufaisha kimapato wakazi wa Igunga

**Tabora**

**ALLAN KITWE NA ABDALLAH AMIR**

WANANCHI wilayani Igunga mkoani Tabora wameshauriwa kuanzisha miradi ya ufugaji samaki kwa kuchimba mabwawa katika maeneo yao ili waweze kujiongezea kipato badala ya kutegemea ajira za serikali.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Ofisa Mfawidhi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Majini katika Skimu ya Umwagiliaji ya Mwamapuli iliyoko wilayani humu, Joachim John, wakati wa zoezi la uvunaji samaki aina ya kambale katika Bwawa la samaki la Ofisa Biashara wa wilaya hiyo, Anthony Marco.

Alisema mradi huo hauna gharama kubwa na kubainisha kuwa mwananchi akitenga eneo la kuchimba bwawa katika eneo analoishi ndani ya mwaka mmoja ataanza kujipatia fedha kwa kuuza kitoweo hicho.

John alibainisha kuwa kituo hicho cha Ukuzaji Viumbe Majini kilichopo katika skimu hiyo kina vifaranga vya samaki vya kutosha ambavyo ni vya aina mbili Kambale na Sato na kifaranga kimoja kinauzwa kuanzia sh. 100 hadi 150.

Alifafanua kuwa kituo chao kimekuwa kikitoa elimu bure kwa wanaotaka kufuga samaki, hivyo alishauri wakazi wa wilaya hiyo na mkoa mzima wa Tabora kuchangamkia fursa hiyo na kuacha kutegemea kazi moja tu ya kilimo.

Mmoja wa vijana wanaofanya kazi katika kituo hicho, Julius Mussa, alisema ufugaji wa samaki ni mzuri kwani unatoa kipato kikubwa kwa muda mfupi ila alibainisha changamoto yao kubwa kuwa ni mitaji, hivyo aliomba asilimia 10 ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri itolewe kwa vijana wote.

Ofisa Biashara wa halmashauri hiyo ambaye pia ni mfugaji samaki, Anthony Marco, alisema aliamua kuchimba bwawa katika eneo lake la makazi na kufuga samaki kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria baada ya kuona kwenye mitandao na majarida yakionyesha faida ya ufugaji wa samaki.

Alisema mwaka mmoja uliopita alichimba bwawa nyumbani kwake Mtaa wa Masanga mjini Igunga na kununua vifaranga 2600 vya samaki aina ya kambale na sato 400 na kuwa sasa ameanza kuvuna na kupata mafanikio makubwa.

Marco alisema maji anayotumia katika bwawa hilo pia anayatumia kumwagilia shamba la lake la vitunguu huku akisema hivi sasa samaki hao wana mwaka mmoja tangu awanunue na kuwafuga.

Alisema vifaranga wamekuwa wakubwa na kila kimoja anauza kati ya sh 3,000 hadi 10,000 kutokana na ukubwa wake.

Alibainisha kuwa kwa sasa anatafuta eneo kubwa vijijini ili aweze kuchimba mabwawa makubwa kwa lengo la kupanua mradi wake na hii ni baada ya kubaini faida kubwa iliyopo katika mradi huo.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kujikita katika kilimo cha nyasi

**Meatu**
**NA ANITA BALINGILAKI**

SERIKALI mkoani Simiyu imewataka wafugaji kujikita katika kilimo cha nyasi kuhakikisha mifugo yao inapata chakula cha uhakika.

Wito huo umetolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, wakati akizungumza na wafugaji wilayani Meatu ambapo alisema kuna faida kubwa kwa wafugaji kufuga kisasa kwa kuzalisha nyasi za malisho.

Alisema serikali inataka wafugaji wapate tija katika mifugo yao na ndio maana inaendelea kuwaelimisha ili kuondokana na ufugaji wa mazoea.

Naye, Ofisa Mifugo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Hussein Nyenye, aliwataka wafugaji kuwa tayari kuingia katika kilimo cha nyasi kwa manufaa ya mifugo yao.

Aliongeza kuwa miaka ya nyuma halmashauri hiyo iliwahi kuleta nyasi za mifugo kisha kuzigawa bure lakini walijitokeza baadhi ya wafugaji wachache kutoitikia kulima kilimo hicho tofauti na sasa ambapo mwitikio umeanza kuonekana kuwa mkubwa.

Nyenye alibainisha kwamba tayari halmashauri hiyo ina mashamba darasa katika maeneo tofauti wilayani hapo ambayo yatawasaidia wafugaji ambao bado hawajaanza kulima nyasi hizo kujifunza.

Mfugaji wa ng'ombe Msanja John, alisema kuna umuhimu kwa wafugaji kupewa elimu ya kutosha kuhusu ufugaji wa nyasi hizo kwani maeneo mengi kwa sasa yamekuwa yakikosa nyasi kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema kilimo hicho kitakuwa muarobaini wa changamoto ya malisho na kuingia katika maeneo ya hifadhi kutafuta malisho.

**Ofisa Mifugo**

Miaka ya nyuma halmashauri hiyo iliwahi kuleta nyasi za mifugo kisha kuzigawa bure lakini walijitokeza baadhi ya wafugaji wachache kutoitikia kulima kilimo hicho tofauti na sasa ambapo mwitikio umeanza kuonekana kuwa mkubwa.

Scanned with CamScanner

UHURU
MAONI YA MHARIRI

# Wafugaji wajikite kilimo cha nyasi kuepusha migogoro

SERIKALI mkoani Simiyu imewataka wafugaji kujikita katika kilimo cha nyasi ili kuhakikisha mifugo yao inapata chakula cha uhakika.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, wakati akizungumza na wafugaji wilayani Meatu ambapo alisema kuna faida kubwa kwa wafugaji kufuga kisasa kwa kuzalisha nyasi za malisho.

Alisema serikali inataka wafugaji wapate tija katika mifugo yao na ndio maana inaendelea kuwaelimisha ili kuondokana na ufugaji wa mazoea.

Hatua iliyotangazwa kuchukuliwa na wafugaji mkoani Simiyu inapaswa kuchukuliwa na wafugaji wote nchini ili mbali ya kuboresha mifugo yao waweze kuepusha migogoro na wakulima.

Hakuna ubishi kuwa migogoro ya wafugaji na wakulima katika maeneo mbalimbali hapa nchini imesababisha madhara makubwa ikiwemo baadhi ya watu kupoteza maisha na wengine kujeruhiwa.

Mbali ya migogoro hiyo, suala la uhaba wa malisho ya mifugo limesababisha baadhi kudhoofika na kufanya kukosa soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Ikumbukwe kuwa miaka iliyopita kuliwahi kuletwa nyasi za mifugo kisha kugawiwa bure, lakini walijitokeza baadhi ya wafugaji wachache kutoitikia kulima kilimo hicho tofauti na sasa ambapo mwitikio umeanza kuonekana kuwa mkubwa.

Tayari, baadhi ya halmashauri zina mashamba darasa katika maeneo tofauti ambayo yanawasaidia wafugaji ambao bado hawajaanza kulima nyasi hizo kujifunza.

Ni dhahiri kuwa kuna umuhimu kwa wafugaji kupewa elimu ya kutosha kuhusu ufugaji wa nyasi hizo kwani maeneo mengi kwa sasa yamekuwa yakikosa nyasi kwa sababu ya mabadiliko ya tabia nchi.

Ndiyo maana tunaunga mkono jitihada zote za serikali zinazofanyika ili kuhamasisha wafugaji katika kushiriki kwenye kilimo cha nyasi ambacho mbali ya kunufaisha mifugo, kitaepusha migogoro ya mara kwa mara baina yao na wakulima.

Uhuru Media Group (UMG)

Scanned with CamScanner